








Mwanzo wa huzuni wa mtu


Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Mwanzo 3-6

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."
Zaburi 119:130

# Mwanzo wa huzuni wa mtu



Kimeandikwa na Edward Hughes
Kimeorodheshwa na Byron Unger; Lazarus

Kimetafsiriwa na Grace Chepkoech
Imerekebishwa na M. Maillot; Tammy S.

Hadithi 2 baadhi ya 60

**M1914.org**

**Bible for Children, PO Box 3, Winnipeg MB R3C 2G1 Canada**

Leseni: Unahaki ya kunakili au kuchapisha hadithi hii. Mradi tu.

**Mungu anajua** kuwa tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Mshahara wa dhambi ni mauti.

**Mungu anatupenda** sana hadi akamtuma mwana wake, Yesu, aje afe msalabani na alipe mshahara ule wa dhambi. **Yesu alifufuka** na akarudi mbinguni! Sasa Mungu anaweza kusamehe dhambi zetu.


**Kama unataka kuondoka kwa dhambi zako,** mwambie Mungu haya: Mungu mpendwa, ninaamini kuwa Yesu alikufa kwa ajili yangu na anishi tena. Tafadhali njoo maishani mwangu na usamehe dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya na niwe nawe milele. Nisaidie niishi kwako kama mtoto wako. Yohana 3:16

**Soma bibilia na zungumza na Mungu kila siku!**

Kiswahili Swahili







"Mungu aliwaamri msile matunda ya miti yote, sivyo?" nyoka akamwuliza Hawa. "Tunaweza kula matunda ya miti yote ila moja," Hawa akajibu. "Tukila tunda la hilo mti, tutakufa." "Hamtakufa," nyoka akamdanganya.
3
"Mtakuwa kama Mungu." Sasa Hawa akatamani tunda la huo mti aliokatazwa na Mungu. Alimsikiza nyoka na akala tunda lile.
4
Baada ya Hawa kutomtii Mungu, alimuongoza Adamu naye pia akala lile tunda. Adamu alitakikana kumueleza Hawa, "La! Sitakubali kutotii neno la Mungu."
5
Baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi, walikuja kugundua kuwa walikuwa uchi. Kwa hivyo, wakashona matawi ya miti kuwa mavazi na kujificha ndani ya misitu kutokana na uwepo wa Mungu.
6
Katika barizi ya jioni, Mungu akaja shambani. Alijua kuwa Adamu na hawa walikuwa wametenda dhambi. Adamu alimlaumu Hawa. Hawa alimlaumu nyoka. Mungu akasema, "Nyoka amelaaniwa. Mwanamke pia atapitia machungu anapozaa watoto." "Adamu, Kwa vile umetenda dhambi, ardhi imelaaniwa na miiba. Binadamu atalima na kutoa jasho ndipo apate chakula."
7
Mungu akawatoa Adamu na hawa nje ya bustani lile zuri. Kwasababu walitenda dhambi, walitenganishwa na Mungu mwenye uhai!
8
Mungu akatengeneza upanga wa moto wa kutunza Bustani la Edeni. Pia Mungu akawatengenezea Adamu na Hawa mavazi kutokana na ngozi. Mungu alitoa ngozi wapi?
9
Kwa wakati, familia ikazaliwa kwa Adamu na Hawa. Mwana wao wa kwanza Kaini, alikuwa mkulima. Mwana wao wa pili, Habili, alikuwa mchungaji wa wanyama.
10
Siku moja Kaini alimletea Mungu mimea ya shamba kama sadaka. Habili akamletea kondoo wake mzuri zaidi ya wote kama sadaka. Mungu alifurahia sadaka ya Habili.
11
Mungu hakufurahia sadaka ya kaini. Kwa hivyo Kaini akawa na hasira. Lakini Mungu akasema, "Ukitenda kile kilicho sawa utakubaliwa, sivyo?"
12
Hasira ya Kaini ikazidi kumpanda. Baada ya wakati usio mrefu alimvamia nduguye Habili – na akamwua!
13
Mungu akamzungumzia Kaini. "Yuko wapi ndugu yako Habili?" "Sijui," Kaini akadanganya. "Mimi ni mwekaji ndugu yangu?" Mungu akamwadhibu Kaini kwa kumnyang'anya uwezo wake wa ukulima na kumfanya awe mtu anayezurura ovyo.
14
Kaini aliondoka kutoka uwepo wa Mwenyezi Mungu. Akamwoa binti wa Adamu na Hawa. Hapo wakakuza jamii. Katika wakati usio mrefu, wajukuu na vitukuu wa Kaini wakajaza mji ambao aliuanzisha.
15
Wakati huo huo, familia ya Adamu na Hawa ikazidi kuongezeka.
16
Wakati mwana wake Sethi alizaliwa, Hawa akasema, "Mungu amenipa Sethi kwa nafasi ya Habili." Sethi alikuwa mcha Mungu aliyeishi miaka 912 na akawa na watoto wengi.
17
Duniani, watu walizidi kuwa waovu vizazi vilivyoendelea kuongezeka. Mwishowe, Mungu akaamua kuwaangamiza wanadamu na wanyama wote na ndege.
18